



BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA TISA

Kikao cha Kwanza – Tarehe 7 Februari, 2018.

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

- I. **TAARIFA YA SPIKA:**

- II. **HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

Nakala zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 16 Disemba, 2017.

Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Kusimamia Mwenendo wa Biashara na kumlinda Mtumiaji ya Zanzibar Nam. 2 ya Mwaka 1995 na Kutunga Sheria Mpya ya Ushindani Halali wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji, Kuweka Masharti Bora Zaidi Pamoja na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Kusimamia Mwenendo wa Biashara na kumlinda Mtumiaji ya Zanzibar Nam. 2 ya Mwaka 1995 na Kutunga Sheria Mpya ya Ushindani Halali wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji, Kuweka Masharti Bora Zaidi Pamoja na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

III. MASWALI:

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

74. MHE. SIMAI MOHAMED SAID (Jimbo la Tunguu) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais

Kwa kuwa nchi ya Qatar na wananchi wake wanatafuta fursa za kibiashara kutoka nchi tofauti.

Je, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haioni umuhimu wa kufungua ubalozi mdogo hapa (Consulate General) kwa ajili ya kushawishi wafanyabiashara tofauti.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

69. MHE. SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Serikali inastahiki pongezi katika juhudi zake za kuleta maendeleo na kuboresha mambo mbali mbali nchini, hata hivyo, ili kuendana na wakati katika sehemu ambazo ujenzi wa majengo unaendelea huwekwa bao la kuonesha jengo hilo ni la nani na madhumuni yake nini na mwisho huwa kuna maandishi (H.I.V) ya Ukimwi na nembo hiyo huwa kama ndio kibali cha ujenzi na kama ni maradhi yanayotukabili hapa Zanzibar.

- (a) Je, maandishi hayo ya (H.I.V) ni lazima yaandikwe ndio upate kibali cha ujenzi.
- (b) Je, kuna malipo yanayolipwa kwa ajili ya matangazo hayo.
- (c) Je, kama ni janga mbona yapo majanga mengi kama malaria, kipindupindu na huwa hayaandikwi.

Wizara ya Elimu Na Mafunzo ya Amali:

58. MHE. SAID OMAR SAID (Jimbo la Wingwi) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar katika mfululizo wake wa kuendeleza ujenzi wa Madarasa ya kusomea, ilijenga banda lenye jumla ya madarasa matano katika skuli ya Sizini mnamo mwaka 2010 ambalo hadi leo hii halijaezekwa.

Je, Mhe. Waziri unawapa matumaini gani wananchi wa Sizini kutokana na kilio chao cha muda mrefu juu ya banda hili ili watoto wao waweze kulitumia kabla ya kuanguka.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

1. MHE. OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

- (a) Je, nini hatma ya Kampuni ya ujenzi ya SHPYA ambayo ilipewa kazi ya kujenga barabara zetu lakini ikashindwa kuendelea na kazi na kufanya barabara hizo zisiendeleee kutengezwa.
- (b) Je, Serikali ilipata hasara kiasi gani kutokana na Mkandarasi huyo kushindwa kufanya kazi kama ilivyokusudiwa.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko:

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Kusimamia Mwenendo wa Biashara na kumlinda Mtumiaji ya Zanzibar Nam. 2 ya Mwaka 1995 na Kutunga Sheria Mpya ya Ushindani Halali wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji, Kuweka Masharti Bora Zaidi Pamoja na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo – Kusomwa kwa Mara ya Pili.

Zanzibar,
7 Februari, 2018.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.